


KANISA LAKO LAWEZA KUKUA

na
Boyd Pearce



KANISA LAKO LAWEZA KUKUA



na
Boyd Pearce

•
Copyright, 1984
International Publications Services
All rights reserved

Published by
International Publications Services

Printed by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi

YALIYOMO

SOMO

UKURASA

1. KUSUDI LA SHULE YA JUMAPILI	5
2. KUTAYARISHA SHAMBA	9
3. UTARATIBU WA SHULE YA JUMAPILI	11
4. HATUA ZA KWANZA ZA SHULE YA JUMAPILI NZURI	18
5. KUPANGA SHULE YA JUMAPILI YAKO	24
6. KUTUMIA SHULE YA JUMAPILI KUWAFIKIA WATU	30
7. MWALIMU WA SHULE YA JUMAPILI	34



KUSUDI LA SHULE YA JUMAPILI

Wachungaji na viongozi wengine wanataka makanisa yao yakue na kusitawi. Wanataka kuwafikia watu wa jamii zao ili wawavute kwa Kristo. Wanataka washiriki wa makanisa wakomae katika imani yao. Mara nyingi hawafahamu jinsi wawezavyo kufanya ili kuzitimiza shabaha hizo. Wanahitaji mpango ambao utasaidia kuyasitawisha makanisa.

Kusudi la kitabu hiki ni kueleza ya kwamba Shule ya Jumapili ndiyo huo mpango unaohitajiwa na makanisa. Shule ya Jumapili thabiti inaweza kusaidia hata kanisa dogo likue. Kanisa laweza na tena ni lazima litumie Shule ya Jumapili yake kuwafundisha washiriki wake jinsi ya kuwafikia jamii. Bila Shule ya Jumapili thabiti kanisa haliwezi kutimiza hata moja ya mambo hayo kwa njia ifaayo.

Kanisa lahitaji Shule ya Jumapili thabiti ambayo imepangwa vizuri. Kitabu hiki kitaeleza jinsi jambo hilo lilivyo la muhimu, jinsi ya kupanga na baraka zitakazopatikana kwa kanisa.

1. Kwanza, Shule ya Jumapili ni nini?

A. Shule ya Jumapili ni watu - watu wote: washiriki wa kanisa, watu wasioamini, Wakristo ambao hawahudhuria ibada za kanisa, watu wote wa jamii. Ni ya watu wazima na vijana na watoto.

B. Wanaohudhuria hugawanywa katika makundi madogo madogo yaani madarasa. Wanagawanywa kulingana na umri wao, ili pawe na darasa kwa kila mtu wa jamaa.

C. Makundi madogo au madarasa huwezesha Shule ya Jumapili kutimiza mambo mawili. Kwanza, mwalimu anaweza kufundisha vyema kundi dogo. Pili, kundi dogo laweza kufanya kazi vizuri zaidi kanisani na kwa jamii.

2. Kusudi la Shule ya Jumapili ni nini?

Kusudi la msingi wa Shule ya Jumapili ni kuwavuta watu kwa Kristo na kanisani. Hilo limekuwa lengo la Shule ya Jumapili wakati wote. Shabaha ya Shule ya Jumapili ni "Kuunganisha" washiriki wa kanisa ili waeneze Injili kwa jamii. "Kuunganisha" ina maana ya "kuwakusanya watu pamoja kwa kazi." Maana yake ni kuwatayarisha, kuwatia moyo, kuwachochea, kuwatia bidii, kuwawezesha ili waende nje


na kuwavuta kanisani watu wa jamii. Washiriki wa kanisa ni lazima waunganishwe waeneze Injili kwa jamii jirani. Hili ni kusudi la Shule ya Jumapili.

3. Ni nini wajibu au kazi ya Shule ya Jumapili?

A. KUWAFIKIA watu wa jamii kwa masomo ya Biblia. Ni lazima Shule ya Jumapili iwafikie watu wote. Asiachwe hata mmoja. Hata ingawa Shule ya Jumapili imepangwa kwa taratibu njema haitaweza kuongezeka ikiwa waalimu wake na wanafunzi hawatoki nje kuwatafuta watu. Itajisifu ikiridhika ilivyo yenyewe na itashindwa kutimiza ule wajibu wake ulio mkuu.

B. KUWAFUNDISHA watu Biblia. Mafundisho ya Biblia ni msingi ambapo Shule ya Jumapili imejengwa. Ni lazima Shule ya Jumapili iwavute watu wa jamii na kuwafundisha Neno la Mungu. Ni kazi ya Shule ya Jumapili kufundisha Biblia katika kila darasa, iwe ni darasa la watoto wadogo au la watu wazima. Hata watoto wadogo wanaweza kufahamu mambo mengi ya mafundisho ya Biblia.

Neno hili, "Shule ya Jumapili" lina maana ya shule inayokutana siku ya Jumapili. Ni shule ya kanisa. Kitabu cha mafundisho ni Biblia. Wajibu ni kufundisha Biblia. Yampasa kila mmoja ahudhurie Shule ya Jumapili. Mara nyingi watu wazima husema ati Shule ya Jumapili ni mafundisho ya watoto wadogo pekee. Je! hilo ni kweli? Ni kufikia umri gani mtu humaliza kujifunza mafundisho yote ya Biblia? Ikiwa ni rahisi kuwashawishi watu wazima wahudhurie madarasa ya Shule ya Jumapili kwa kutumia jina lingine badala ya Shule ya Jumapili, basi washawishi kwa njia hiyo. Yaite madarasa yao "madarasa ya Biblia" au "masomo ya Biblia." Jambo muhimu ni kwamba kanisa liwe na mpango wa kufundisha Biblia kwa makundi ya kila umri.



C. KUWAVUTA watu wamwamini Kristo na kuwaongoza wawe washiriki wa kanisa. Haitoshi kuwafikia watu na kuwafundisha tu. Ni lazima Shule ya Jumapili ikamilishe kazi yake. Ni lazima kuwatafuta wenye dhambi na kuwavuta wamwamini Kristo. Hii ni kazi ya kila mshiriki wa kanisa.

D. KUWAKUZA Wakristo wakomae kama watumishi wa Bwana. Huu ndiyo wajibu muhimu wa Shule ya Jumapili. Biblia humfananisha mtu aliyeokolewa na mtoto mchanga kirohoni. Ni lazima akue na aweza kufanya hivyo kwa njia tatu.

1. Kwanza, anakua kwa Neno la Mungu. Ni lazima afundishwe. Biblia humfunza habari ya maisha yake ya imani. Agano Jipya halitofautishi kati ya kukua katika neema na kukua katika hekima. Ni lazima washiriki wa kanisa wafundishwe Biblia ili wakue. Shule ya Jumapili ndiyo mpango wetu wa kutimiza wajibu huo.

2. Pili, Wakristo hukua kwa utumishi, wakitumika kanisani. Ni lazima Mkristo amtumikie Bwana ili akue. Ni lazima ajifunze kutumikia. Ni lazima awe na nafasi za kufanya kazi fulani kanisani. Nafasi kama hizo hupatikana katika Shule ya Jumapili. Katika madarasa yao, yawapasa Wakristo wajifunze kutembelea watu na kushuhudia, kuongoza na kufundisha, kuwaomba wengine na kuwasaidia watu katika shida zao. Ni shabaha yetu kuwakuza washiriki waishi maisha yaliyo mfano wa Kristo ya utumishi na huduma. Shule ya Jumapili husaidia kanisa kutimiza wajibu huo.

3. Tatu, Wakristo hukua kwa uhusiano wao na Bwana. Hufundishwa zaidi habari ya Biblia. Wanajishughulisha na kazi ya Bwana. Wanajifunza, kumtegemea Bwana. Ushirika wao na Kristo huongezeka kina. Wanajifunza kuomba na kuufurahia ushirika wa Wakristo wengine waaminifu katika darasa lao la Shule ya Jumapili.

Shule ya Jumapili thabiti ni msaada mkubwa kwa mchungaji. Inawasaidia washiriki wa kanisa kukua katika maisha yao ya Kikristo.



E. KUWAHUDUMIA

watu wenye shida. "Kuhudumu" maana yake ni kuwahurumia na kusaidia. Kuhudumu katika jamii ni kazi ya kila darasa la Shule ya Jumapili. Kila kundi laweza kufahamishwa mahitaji ya jamii na wanafunzi wa darasa lake. Kwa hivyo wanaweza kuwahudumia watu walio na mahitaji.



Yampasa mwalimu wa Shule ya Jumapili azifahamu shida za wanafunzi wake. Ndipo ataweza kuzitatua shida hizo wakati anapofundisha Biblia.

KUWAFIKIA! KUWAFUNDISHA! KUWAVUTA! KUWAKUZA! KUWAHUDUMIA! Hizi ni kazi za Shule ya Jumapili. Ni lazima kanisa lizifanye ili kutimiza wajibu wake kama kanisa. Shule ya Jumapili hutokeza mafanikio. Inaweza kusaidia kanisa likue na kufaulu kwa njia lililoweza kufaulu kwa njia nyingine.

Hata hivyo, ni lazima ifahamike ya kwamba kuwa na Shule ya Jumapili ni jambo gumu. Makanisa mengine hushindwa kuwa na Shule ya Jumapili kwa sababu hayaelewi na jambo hilo. Yanafikiria ati baada ya kuanzisha madarasa mawili au matatu na kumpata mwalimu kwa kila darasa na kuwapatia vitabu vya mafundisho, kazi yao imetimilika. Baada ya hivyo wanalegea kwani wanayo Shule ya Jumapili! Baadaye wanastaajabu kugundua ya kwamba watu hawapendezwi na Shule ya Jumapili yao. Haitimizi jambo lo lote. Hawajafahamu ya kwamba ni lazima kuendelea kutia juhudi kulea Shule ya Jumapili iwe nzuri. Kuwafundisha na kuwazoeza waalimu ni jambo la lazima mwaka baada ya mwaka.

Ni lazima Shule ya Jumapili kutimiza kusudi lake kuu na kuzifanya kazi zake muhimu tano. Ni kazi gumu! Lakini ingawa ni kazi gumu, ni lazima ifanywe. Kweli, kanisa haliwezi kufaulu bila Shule ya Jumapili thabiti. Usiogope kazi gumu. Fikiria mambo ambayo Shule ya Jumapili itaisaidia kanisa lifaidike kwalo na tia bidii.

KUTAYARISHA SHAMBA

Kabla ya kupanda mbegu mchangani ni lazima kuanza na matayarisho ya mchanga. Yampasa mpanzi achimbue mchanga na kuondoa kwekwe. Vivyo hivyo ni lazima pawe na matayarisho kabla ya kuwa na Shule ya Jumapili.

Ili kanisa liwe na Shule ya Jumapili thabiti ni lazima lielewe na taratibu ya kanisa la Agano Jipya na kazi yake. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba makanisa mengi yanafifia kwa sababu hayaelewi na taratibu au kazi yake. Hayaelewi na mpango wa Shule ya Jumapili kwa sababu hayajakubali jinsi kanisa lao linavyopaswa kuwa. Ni lazima kazi ya kanisa la Agano Jipya ifahamike kabla ya kuwa na Shule ya Jumapili.



Katika Agano Jipya, mara nyingi Paulo amefananisha kanisa na mwili. Soma kwa makini 1 Wakorintho 12:12-27. Isome mara kadha na ujaribu kuelewa jinsi maandiko hayo yasemavyo juu ya kanisa. Kanisa ni kama mwili. Mwili una viungo vingi, na kila kiungo ni cha muhimu mwilini mwote. Kila kiungo cha mwili kina kazi yake.

Washiriki wa kanisa ni kama viungo mbalimbali vya mwili. Hiyo ina maana ya kwamba kila mmoja ni muhimu; hakuna mshiriki asiye muhimu kanisani. Kichwa cha mwili ni Yesu Kristo mwenyewe (Wacفسo 1:22-23). Anavipa viungo mbalimbali vya mwili kazi ambayo anataka vifanye. Anauambia mwili mzima kazi upasayo uifanye. Kanisa hutimiza kazi yake kubwa ikiwa washiriki wote wanafanya kazi zao.

Hii inahusu mambo matatu kanisani:

1. Ina maana ya kwamba kila mshiriki wa kanisa anayo kazi ya kufanya. Ikiwa viungo fulani vya mwili havifanyi kazi, basi mwili hautimiza kazi yake ipasavyo. Ni muhimu kwa kila kiungo cha mwili kifanye kazi yake. Vile vile, kila mshiriki wa kanisa yampasa afanye kazi yake. Makanisa mengi siku hizi yanafifia kwa sababu hayajafahamu jambo hili. Yanawaacha washiriki wake wakae bila kufanya kazi. Kazi yote ya kanisa inafanywa na washiriki wachache tu. Kitendo hicho ni kinyume cha mpango wa Bwana wetu kwa kanisa lake. Kanisa ni kama

mwili! Kila kiungo cha mwili kinayo kazi ya kufanya. Ikiwa kanisa litafaulu ni lazima washiriki wote wafanye kazi. Kanisa haliwezi kuwa na Shule ya Jumapili imara mpaka lielewe na jambo hili. Shule ya Jumapili ni juhudi ya kanisa zima. Inahitaji usimamizi na msaada wa kila mshiriki ili iweze kutimiza wajibu wake.

2. Kanisa kama mwili ina maana ya kwamba kila mshiriki anapewa kazi fulani afanye. Haitoshi kusema ati yampasa kila mshiriki wa kanisa afanye kazi. Macho yanayo kazi fulani ya kufanya mwilini. Miguu inayo kazi fulani ya kufanya. Kila mshiriki wa kanisa ni lazima afanye kazi fulani ambayo ametengewa na kutayarishwa na Kristo kuifanya. Kwa mfano, mshiriki mmoja hawezi kuamua binafsi ya kwamba ataanza kufundisha darasa la watu wazima, au mwingine aamue ya kwamba atafundisha darasa la vijana. Kadhalika, mshiriki hawezi kusema, "Kwa sababu sijapewa kazi ya kufundisha, sitafanya kazi nyingine yo yote." Yesu Kristo ni kichwa cha kanisa. Anaamua ni washiriki wangapi watakaokuwa waalimu, na anawapa vipawa vya kutimiza kazi hii. Ikiwa tunayaamini mafundisho ya Agano Jipya, ni lazima kuamini ya kwamba kwa kila kazi Bwana atakayo ifanywe kanisani, atamchagua mtu fulani kuifanya kazi hiyo. Ikiwa kanisa litawatafuta kwa njia ya maombi wale ambao wamechaguliwa na kupewa vipawa na Kichwa, basi kutapatikana waalimu wa kutosha na wafanyi kazi wa Shule ya Jumapili kwa njia ifaayo.

3. Kanisa kama mwili ina maana ya kwamba washiriki wote wa kanisa wafanye kazi pamoja wakiwa na umoja. Kila mmoja afanye kazi ili kanisa liweze kutimiza wajibu wake mkuu. Jambo moja la maana ya mwili wa mwanadamu ni kwamba kichwa kikiamua ni kazi gani mwili utafanya, viungo vyote vya mwili hushirikiana kutimiza kazi hiyo. Kama kichwa kikisema, "Tembea", mwili wote hutembea. Miguu, mikono, macho, masikio - kila kiungo cha mwili hufanya kazi pamoja, kila kimoja kikifanya kazi yake kutimiza lengo la kutembea. Hii ndiyo njia ipasayo kanisa kufanya kazi yake. Panapo kazi ya kufanywa, na kila mshiriki anatumia vipawa vyake na kufanya kazi yake, basi watafaulu. Lakini lazima wafanye kazi pamoja wakiwa na umoja kama vile mwili ufanyavyo kazi. Katika Shule ya Jumapili kila mshiriki wa kanisa atakuwa na kazi ya kufanya. Ikiwa kila mmoja atafanya kazi yake, basi Shule ya Jumapili itafaulu.

Hakikisha ya kwamba kanisa linafanya kazi kama Kristo alivyokusudia. Ni lazima kanisa zima lifanye kazi pamoja ili litimize shabaha yake. Ikiwa kanisa limefahamu jambo hilo, basi ardhi itakuwa tayari kupanda mbegu ya Shule ya Jumapili thabiti.

UTARATIBU WA SHULE YA JUMAPILI

Kabla mtu hajajenga nyumba shambani mwake, yamlazimu kwanza achimbe mashimo na kutia nguzo ndani. Baadaye hujaza mashimo mchanga na mawe na labda saruji ili kushikilia nguzo ziwe imara ardhini. Halafu hupigilia misumari au kufunga kamba zito kwa nguzo ndipo nyumba huanza kuwa na umbo lake. Huu ni muundo au kiunzi cha nyumba. Ni kitu cha maana sana kwani nyumba inajengwa kwa muundo huo.



Pia, muundo ni kitu cha maana katika kujenga Shule ya Jumapili. Ni lazima muundo utengenezwe ambapo Shule ya Jumapili itajengwa. Muundo huu ni utaratibu wa Shule ya Jumapili.

Ni lazima taratibu ipangwe kwa migawo minne ya umri tofauti tofauti.

MGAWO WA WATOTO WADOGO

Mgawo huu ni wa watoto wadogo. Ni watoto ambao hawajaanza kwenda shule. Ni jambo la muhimu ya kwamba watoto hao wajifunze Biblia. Wakutanapo wamepaswa kutimiza zaidi kuliko kupigishwe makofi, kuimba na kuambiwa hadithi rahisi tu. Ni lazima wafundishwe. Biblia hufundisha ukweli huu. Nyakati za Agano la Kale, Mungu aliwaamuru watu wake kuwafundisha watoto wao. Soma Kumbukumbu la Torati 4:9. Mafundisho ya watoto yalifanyika nyumbani. Walakini katika Nehemia 12:42 tunasoma pia ya kwamba watoto walihudhuria ibada za hekalu na wakafundishwa humo. Timotheo ni mfano wa manufaa wa kumfundisha mtoto. Mama yake na nyanya yake walimfundisha (2 Timotheo 1:5 na 3:15). Vile vile alihudhuria sinagogi, na kiongozi alimfundisha.

Jina la darasa hili la kwanza ni “Watoto Wadogo”. Ni watoto ambao wameanza tu kujifunza. Umri wa watoto hao ni kutoka miaka minne mpaka miaka sita. Kama kanisa halina chumba cha watoto wadogo sana, mtoto wa miaka mitatu au chini yake angekaa na mama yake. Huyu ni mdogo sana, asiweze kujifunza pamoja na watoto walio wakubwa. Kama akikaa pamoja nao huenda atawazuia wasifundishwe vyema.

Watoto Wadogo ni wa tabia gani?

1. Ni mtukutu na mtendaji mwepesi sana. Anaweza kukaa kimya na kusikiliza kwa dakika 5-10 tu. Ni lazima awe na tendo la kufanya.

2. Hupenda kuiga na kukariri. Hujifunza kwa njia ya kuiga wengine, akifanya wafanyavyo na kukariri wasemavyo. Watoto wadogo si wasomaji. Kwa hivyo kuiga na kukariri ni njia nzuri za kuwafundisha.

3. Ni mchunguzi sana. Anataka kuona, kusikia, kugusa na kuonja kila kitu.

4. Anaweza kuelewa kama “ajifikiriaje binafsi”. Amejawa na wazo la “mimi”. Maneno atumiayo kwa wingi sana ni “yangu”, na “mimi”.

5. Ingawa ni mtendaji mwepesi sana na mchunguzi ana uwezo kidogo wa kufahamu. Hawezi kuelewa na mawazo kama ya “imani” na “neema”. Lakini anaweza kufahamu jinsi Mungu awezavyo kumsaidia na kuwa pamoja naye kila siku. Ni lazima mwalimu amfundishe kwa njia zinazoweza kumfanya afahamu.

Vifaa vya Kufundisha: Yapasa kanisa limpatie mwalimu masomo ya kufundisha. Masomo haya yanaitwa “Mwalimu wa Watoto” au “Kufundisha Watoto Wadogo”. Kunazo picha za rangi za kufundisha na “picha za watoto” ziwezazo kuchukuliwa nyumbani ambazo hutumiwa pamoja na kitabu cha mwalimu. Kila kitabu kina masomo 13 ya kutosheleza miezi mitatu. Agiza vitabu hivi kutoka kwa Baptist Publishing House.

MGAWO WA VIJANA WADOGO

Mgawo wa pili ni wa vijana wadogo. Watoto wa mgawo huu ni wa umri kutoka miaka saba mpaka miaka kumi na miwili. Shuleni watakuwa wanasoma darasa la kwanza hadi la sita.

Biblia hutufunza kwamba tuchukue wajibu wetu kwa bidii ili tuwafundishe watoto wetu. Twajua ya kwamba watoto wakuavyo, miili na akili zao huongezeka. Basi, hatuna budi kuwagawanya katika makundi kulingana na umri wao na mabadiliko ya uwezo wao wa kufahamu.

Watoto wa mgawo huo wangepiganywa katika madarasa mawili. Wale wa umri wa miaka saba, minane na tisa wawe darasa moja. Darasa hili huitwa “Watoto Wakubwa”. Watoto hao wanahitaji kujengewa msingi mzuri. Tuwafikirie kama wale walio katika hatua zao za kwanza za kukua. Wengi wao watakuwa wameanza kuhudhuria shule; na watakuwa wanajifunza kusoma.

Watoto Wakubwa ni wa tabia gani?

1. Ni mwepesi wa kutenda. Hufurahia kufanya mambo, na hafurahii kukaa kimya kwa muda mrefu.

2. Kama watoto katika darasa la kwanza huyu pia hupenda kuiga. Huanza kuiga nia au hali pamoja na vitendo.

3. Hupendelea kujifunza. Ana shauku na mara huuliza “kwa nini?”

4. Ana bidii ya mawazo. Hupendelea hadithi za vitendo vikielezwa vizuri.

5. Ana mawazo rahisi. Hupendelea mazungumzo. Hupendelea kujibu maswali rahisi. Lakini angali na shida kufahamu mawazo kama “Imani” na “neema”.



6. Anashirikiana. Hutaka kuwapendeza watu wazima.

Vifaa vya Mafundisho: Kuna vitabu vya masomo kwa wanafunzi wa darasa la watoto wakubwa. Kama vitabu hivi havipatikani katika nchi yako, unaweza kutumia kitabu cha “Mwalimu wa Watoto” na picha zao. Kwa sababu watoto hao ni wakubwa wataweza kujifunza vifungu vingi vya kukariri. Unaweza kuwachagulia vifungu vingine vya kujifunza.

Darasa la pili la Mgawo wa Vijana Wadogo ni wa umri wa miaka kumi hadi kumi na miwili. Darasa hili huitwa darasa la Vijana Wadogo. Kijana mdogo afahamike kama mmoja ambaye ameanza kukua ingawa angali katika kiwango cha utoto. Mekanisa mengine yameonelea ni rahisi

madarasa ya Shule ya Jumapili zao zifuate utaratibu wa madarasa ya shule ya kiserikali. Yaani, darasa la Watoto Wadogo litakuwa la watoto ambao hawajafikia umri wa kwenda shule; darasa la Watoto Wakubwa litakuwa la wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu; darasa la Vijana Wadogo ni la wanafunzi wa darasa la nne hadi sita. Taratibu hiyo ni nzuri lakini hujihadhari usimtatize mtoto ambaye ameacha shule. Kama ameacha shule ahudhurie darasa la Shule ya Jumapili la watoto wa umri wake.

Kijana Mdogo ni wa tabia gani?

1. Ni mwepesi wa kutenda. Anaweza kukaa kimya na kusikiliza vema, lakini hupendelea hadithi za vitendo na nyimbo.
2. Huuliza maswali mengi. Hupendelea kujua “jinsi gani?” na “kwa nini?”
3. Ni mshindani. Hupendelea michezo, mafumbo na mashindano.
4. Huweza kukariri upesi.
5. Hupokea Injili kwa urahisi. Kundi la umri huu ni muhimu. Ni katika umri huu watoto wengi humpokea Kristo. Wanahitaji tena wanastahili mafundisho yaliyo bora zaidi na uongozi viwezazo kupatiwa na kanisa.

Vifaa vya Kufundisha: Kuna masomo kwa umri huu. Pamoja na vitabu vya waalimu pia kuna vitabu vya wanafunzi. Kila kitabu kina masomo 13 yatoshayo kwa mafundisho ya miezi mitatu. Vitabu hivi hupatikana kutoka kwa Baptist Publishing House au duka la vitabu la Wabatisti linalotumikia nchi yako. Vitabu hivi huitwa, “Vijana Tujifunze Biblia” (Mwalimu).

MGAWO WA VIJANA (YOUTH)

Huu ndio Mgawo wa tatu wa Shule ya Jumapili. Ni kwa vijana wa umri wa miaka kumi na mitatu hadi ya ishirini. Pia vijana huweza kugawanywa katika madarasa mawili.

Darasa la kwanza ni la vijana wenye umri wa miaka kumi na mitatu hadi kumi na mitano. Darasa hili linaitwa "Vijana". Hawa ni wale walio 'katikati': si watoto na si watu wazima. Huu ni wakati muhimu katika maisha yao.



Uliza habari za vifaa vya kufundisha darasa hili kutoka kwa Baptist Publishing House.

Darasa la pili katika Mgawo wa Vijana ni kwa vijana wa miaka kumi na sita hadi ya miaka ishirini. Darasa hilo linaitwa na jina lake la Kiingereza, "Youth".

Kijana au "Youth" ni wa tabia gani? Huhitaji nini?

1. Vijana huhitaji mwalimu hodari anayejitayarisha vema. Wanahitaji kuchochewa na yale wasikiayo.

2. Hufanya maamuzi mengi juu ya maisha. Huhitaji mwalimu awezaye kusaidia.



3. Hawatapendezwa na hadithi za Biblia au mafundisho isipokuwa wametambua jinsi yahusikavyo na maisha yao ya kila siku. Hupendelea kujadiliana juu ya ukweli wa Biblia kama wakitambua manufaa yahusuyo mambo ya maisha ya ulimwengu wao.

4. Kikundi hiki ni cha manufaa kwa kijana. Kijana huhitaji kuona ya kwamba amekubalika na kikundi chote. Vijana hupendelea kushirikiana pamoja. Mwalimu awapangie mambo ya kufanya katikati ya wiki. Michezo ya kikundi, kwa mfano mpira wa mikono (volleyball) ambao huweza kucheza na wavulana na wasichana pamoja, yafaa sana.

5. Ili kijana aweze kuwa mshiriki mwaminifu wa kanisa awapo mtu mzima, yafaa afundishwe kwa makini wakati wa miaka hiyo muhimu.

Vifaa vya Kufundisha: Vitabu vya masomo ya vijana ni vya muda wa miaka mitano vikiwa vitabu vinne vya masomo kwa kila mwaka. Uliza majina ya vitabu hivyo na viagize kutoka kwa Baptist Publishing House au duka la Vitabu la Wabatisti linalotumikia nchi yako.

Vifaa vingi vya kufundishia kundi la umri huu vimetayarishwa hasa kwa kijana aliye shuleni. Hata hivyo usisahau ya kwamba kunao vijana wengi ambao hawapati nafasi ya kujiunga na shule za sekondari. Hao wasisahauliwe katika kutayarisha na kupanga darasa hili. Tena, katika sehemu nyingine za mashambani vijana wengi wamesafiri wahudhurie shule kwa muda wa miezi tisa au kumi ya mwaka. Na makanisa yao ni lazima kuwafanyia mpango mzuri wanapokuwa nyumbani wiki za likizo.

MGAWO WA WATU WAZIMA

Huu ni Mgawo wa nne wa Shule ya Jumapili. Kwa kawaida vijana huanza kuhudhuria darasa la watu wazima kati ya umri wa miaka kumi na minane hadi ya ishirini na miwili. Mara nyingi kanisa likianzisha Shule ya Jumapili yake litaanza na darasa moja tu la watu wazima. Walakini yapasa ikumbuke ya kwamba itafaa kuligawanya darasa hilo na kuanzisha darasa lingine upesi iwezekanavyo. Madarasa ya watu wazima yaweza kugawanywa kwa njia tatu:



1. Waume kwa wake. Yaani, kuwa na darasa moja la wanaume na lingine la wanawake.

2. Kwa umri. Yaani, kuwa na darasa moja la watu wa makamo wanaume pamoja na wanawake na lingine la wazee wanaume pamoja na wanawake.

3. Labda njia iliyo bora zaidi ni kuyagawanya kulingana na umri na pia wanawake kwa wanaume. Kulingana na wingi wa watu wako wazima uwe na madarasa mawili ya wanaume. Darasa moja la wanaume wa makamo na lingine la wanaume wazee. Tena uwe na madarasa mengine mawili ya wanawake. Darasa moja la wanawake wa makamo na lingine la wanawake wazee.

Mwalimu wa watu wazima yamlazimu ayajue mahitaji ya wanafunzi wake. Yampasa kuwatembelea na kuyatatua matatizo na mahitaji ya wanafunzi anapofundisha.

Sura 6 itaeleza jinsi darasa la watu wazima liwezavyo kupangwa kutembelea na kuwafikia watu ili waitwe kwa Kristo.

***Vifaa vya Mafundisho:* Kunazó vitabu kadhaa vya masomo ya watu wazima. Vitabu vya mwalimu na wanafunzi vyote viwili vinapatikana. Uliza majina yao na uviagize kutoka kwa Baptist Publishing House.**

HATUA ZA KWANZA ZA SHULE YA JUMAPILI NZURI

Ili kanisa liwe na Shule ya Jumapili imara kunazo hatua za lazima kuanzia nazo. Hizi ndizo msingi ambao utaratibu wa Shule ya Jumapili ungejengwa juu yake.

1. Hatua ya kwanza humtegemea mchungaji. Mchungaji ni kiongozi wa kanisa. Kwa sababu hii, yamlazimu aliongoze kanisa lake kusitawisha Shule ya Jumapili. Kazi ya Shule ya Jumapili huanzia na mchungaji.

A. Kwanza, yampasa mchungaji aelewe kanisa ni nini na jinsi lipasavyo kufanya kazi yake (tazama Sura 2). Kwa vile kanisa ni mwili na washiriki wake wote wana kazi ya kufanya, yampasa mchungaji ajitoe kuwaongoza watu wake kutambua na kuyafanya mapenzi ya Mungu. Anazo kazi mbalimbali za kufanya, lakini kazi iliyo muhimu zaidi ni kuwaongoza washiriki kufanya kazi ambayo Mungu awatakia wafanye. Ikiwa atalijenga kanisa ni lazima avitumie vipawa vyote na uwezo wa washiriki wake. Ni lazima awapatie watu wake nafasi za kufanya kazi na kuhudumia kanisa. Ni jambo la kusikitisha ingawa latendeka ya kwamba washiriki wengi hawafanyi kazi makanisani mwao kwa sababu hawajapatiwa nafasi ya kufanya hivyo. Kumbuka ya kwamba Shule ya Jumapili nzuri itawahitaji washiriki wote wafanye kazi pamoja. Ni wajibu wa mchungaji kuwaongoza.

B. Pili, ni lazima mchungaji awe na nia ya kujifunza. Ni lazima ajifunze kusudi kuu na kazi muhimu za Shule ya Jumapili (Tazama Sura 1). Lazima ajifunze jinsi Shule ya Jumapili inavyotungwa na jinsi ipasavyo kuendesha kazi yake. Lazima ajifunze jinsi ya kupanga ili Shule ya Jumapili iweze kukua siku za usoni (kama itakavyoelezwa katika Sura hii). Kutokana na yale aliyojifunza yampasa mchungaji awe na shauku. Ni lazima asadikishwe ya kwamba kanisa lahitaji Shule ya Jumapili na ya kwamba zaidi ya mpango wo wote mwingine Shule ya Jumapili ndiyo itakayolisaidia kanisa kukua.

C. Yampasa mchungaji awafundishe wengine. Yampasa akubali ya kuwa itamlazimu kutumia muda mwingi kuwafundisha waalimu. Waalimu pia ni lazima wafahamu kusudi na wajibu wa kazi ya Shule ya

Jumapili. Wanahitaji kuelewa tangu mwanzo shabaha zitakazotimizwa na madarasa yao. Ni lazima mchungaji awafundishe waalimu jinsi ya kufundisha. Haitoshi kuwapatia tu kitabu cha mafundisho. Ni lazima wiki baada ya wiki kuwasaidia kutatua matatizo ya mafundisho yao. Ni lazima awafundishe kwa njia ya mfano pamoja na mafunzo yake jinsi ya kutembelea na kutoa ushuhuda. Ni lazima awaongoze wakue katika maisha ya maombi na kujitoa kwa Kristo na kanisa lake. Jambo hilo litachukua muda mwingi wa mchungaji, lakini asisahau ya kwamba afanyavyo kazi ya Shule ya Jumapili anafanya kazi ya kanisa. Anapojenga Shule ya Jumapili analijenga kanisa.



D. Yamlazimu mchungaji kulitegemeza Shule ya Jumapili siku ya Jumapili kwa kuhudhuria na kutia moyo. Afike mapema ili kuwasalimia watu wafikapo. Kuwepo kwake ni kuwaambia watu "Shule ya Jumapili ni sehemu muhimu ya ibada yetu ya Jumapili asubuhi. Nimefurahi ya kwamba mmefika kushiriki". Ni wajibu wa mchungaji Jumapili asubuhi kuhudhuria Shule ya Jumapili. Kama hapendi kufanya hivyo labda anahitaji kazi nyingine ambayo haina matakwa mengi kama mchungaji.

E. Ni lazima mchungaji akikumbuke kipindi cha Shule ya Jumapili anapopanga ibada. Mara nyingi ibada ni ndefu sana. Ikiwa ibada ni ndefu sana hupoteza manufaa mema. Punguza ibada kidogo, ukifahamu ya kwamba watu wametangulia kukaa katika madarasa yao ya Biblia kwa muda wa saa moja.

2. Kama hatua ya pili makanisa mengi humchagua mshiriki mmoja wa kanisa atumike kama msimamizi wa Shule ya Jumapili. Katika kanisa dogo pengine mchungaji anaweza kuwa msimamizi wa Shule ya Jumapili. Katika kanisa kubwa itakuwa msaada kwa mchungaji na waalimu wa Shule ya Jumapili kama mtu mmoja akichaguliwa kutumika kama msimamizi.

Msimamizi wa Shule ya Jumapili angekuwa mtu ambaye amekuwa mwahimu wa Shule ya Jumapili. Mambo mengi yaliyotajwa juu ya mchungaji katika Shule ya Jumapili yanamhusu msimamizi wa Shule ya Jumapili. Yampasa aelewe na mpango wa kazi ya Shule ya Jumapili. Ni lazima afahamu shabaha za Shule ya Jumapili na jinsi kanisa lake liewazavyo kuritimiza. Ni lazima awe Mkristo aliyekomaa na mshiriki mwaminifu wa kanisa.

Wajibu wake utakuwa kusaidia kuwafundisha waalimu, kuwatia moyo, na kuhakikisha ya kwamba kazi inaendelea vema madarasani mwao. Itambidi kufika mapema Jumapili asubuhi na kuhakikisha ya kwamba makao yote ya madarasa yako tayari kwa mafundisho kabla ya Shule ya Jumapili haijaanza. Atahakikisha ya kwamba kuna mwalimu katika kila darasa. Kama mwalimu mmoja amekosa kufika ni lazima msimamizi atafute mtu mwingine wa kufundisha darasa hilo au alifundishe yeye mwenyewe. Msimamizi wa Shule ya Jumapili ashirikiane na mchungaji katika kupanga na kutayarisha Shule ya Jumapili na kuhakikisha ya kwamba inafanya kazi ipasavyo.

Lakini kunalo jambo moja muhimu: Ingawa kanisa huenda likabarikiwa kuwa na msimamizi mwema wa Shule ya Jumapili, jambo hilo halimwondolei mchungaji wajibu wake wote juu ya Shule ya Jumapili.

3. Hatua ya tatu ya kuwa na Shule ya Jumapili nzuri yategemea kanisa lenyewe, kwani kanisa ndilo linalohusika na Shule ya Jumapili yake. Ni lazima kila shule iwe na kundi la watu wanaohusika na mambo ya shule ile. Kwa upande wa Shule ya Jumapili kundi hilo ni kanisa lenyewe. Kanisa lahusika na Shule ya Jumapili kwa njia zifuatazo:

A. Kwanza, kanisa, katika mkutano liamue kuwa na Shule ya Jumapili. Kabla ya kukata shauri, mchungaji awaeleze washiriki kwa makini maana ya Shule ya Jumapili, jinsi iwezavyo kusaidia kujenga kanisa lao na wajibu wa kanisa kwa Shule ya Jumapili. Kama washiriki wakiamua kwamba wanataka Shule ya Jumapili kanisani mwao, wataweza kufahamu kwamba ni Shule ya Jumapili yao na si mpango ulioanzishwa na watu wawili au watatu.

B. Pili, kanisa lahusika na mafundisho yanayofundishwa katika Shule ya Jumapili yake. Mwalimu asiamue peke yake juu ya mafundisho atakayofundisha. Ni lazima kanisa lithibitishe ya kwamba Biblia inafundishwa kwa uaminifu kulingana na kanuni za imani ya Wabatisti. Mpango wa mafundisho wa makanisa ya Kibatisti uko katika vitabu vya masomo vinavyopatikana katika Baptist Publishing House. Vitabu hivi vya masomo vingepatiwa waalimu na kanisa pamoja na maagizo ya kwamba hayo ndiyo mafundisho yatakayofundishwa pekee.

C. Nj wajibu wa kanisa kuwachagua wale watakaofundisha Shule ya Jumapili. Hakuna awezaye kuamua binafsi ya kuwa atakuwa mwalimu wa darasa moja la Shule ya Jumapili. Ni lazima waalimu wachaguliwe na kutengewa kazi na kanisa. Watachaguliwa kufanya kazi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja tu. Wakati mwingine kanisa

litakuwa na mwalimu asiyefaa. Labda ni kwa sababu si mwaminifu au hawezi kufundisha vizuri. Kanisa halijui liwezavyo kumwondoa kama mwalimu. Tatizo hili lingeweza kutatuliwa kama mwalimu angeelewa tangu mwanzo ya kwamba alichaguliwa kutumika kwa kipindi cha mwaka mmoja tu. Kuelekea mwisho wa kila mwaka kanisa lingechagua waalimu wake kwa mwaka ufuatao. Kama mwalimu amekuwa mwaminifu na mwenye kuongoza darasa lake vizuri, anaweza kuchaguliwa kwa kipindi cha mwaka mwingine. Kama mwalimu hakuwa mwaminifu au hana kipawa cha kufundisha angepewa shukrani na kanisa kwa kazi yake aliyokuwa ameifanya lakini aambiwe ya kwamba kanisa limeamua kumchagua mtu mwingine achukue nafasi yake kwa mwaka ufuatao. Waalimu wapya, kama ikiwezekana, wangeanza kazi yao ya kufundisha katika Jumapili ya kwanza ya mwaka mpya.

Kuna dokezo lingine juu ya kuchagua waalimu wa Shule ya Jumapili: Mtu asiye Mbatisti na mshiriki asichaguliwe na kanisa. Kuna Wakristo wazuri na waalimu ambao si Wabatisti au wasiopendelea kujitolea wenyewe kanisani. Labda kanisa likaonelea ya kuwa kwa sababu mtu kama huyo anayo elimu ya kutosha na ni mwalimu aliyefuzu lingebahatika kumchagua awe mwalimu katika kanisa. Labda baadaye kanisa litastaajabu kugundua ya kwamba wale wanaohudhuria darasa lake hawana mawazo ya imani ya Wabatisti. Kama ukitaka kanisa lako lifuate imani yake ya kweli, ni lazima uchague washiriki waaminifu wa kanisa lako wawe waalimu wako.

D. Ni wajibu wa kanisa kutegemeza Shule ya Jumapili kwa fedha. Kanisa lingenunua vitabu vya masomo na vifaa vingine vinavyohitajiwa na Shule ya Jumapili. Waalimu wasinunue vifaa hivyo, na darasa lisichange pesa kununua vifaa hivyo. Lakini ifahamike ya kuwa ingawa ni wajibu wa kanisa kununua vifaa vya kufundisha Shule ya Jumapili, sio wajibu wa kanisa kwa vyo vyote kuwalipa waalimu wa Shule ya Jumapili kwa kazi yao ya kufundisha. Hii ni kazi ya kujitolea ambayo wameikubali kama njia ya kutumikia kanisa na Bwana wao.

4. Hatua ya nne ya kuwa na Shule ya Jumapili nzuri ni kuwa na lengo la kufikia baada ya miaka kadhaa. Jambo hilo lahitaji mawazo mengi na mpango mzuri. Ni lazima uweze kuona ni hali gani ungependelea kanisa lako lifikie. Yakupasa kufahamu uendako na ni jambo gani unatumaini kulitimiza.

A. Kwa mfano, fikiria lengo ambalo kanisa lako lingetimiza kwa muda wa miaka miwili. Jiulize maswali haya: Ungependa kanisa lako liwe na washiriki wangapi baada ya miaka miwili? Ni madarasa mangapi ya Shule ya Jumapili utakayohitaji kuhudumia idadi hiyo ya washiriki?

Ili kujibu swali la kwanza na kuweka lengo lako ni lazima kuelewa na idadi ya watu wanaoishi kuzunguka kanisa lako. Ni jambo la kushangaza ya kuwa kunayo makanisa machache tu yanayofahamu wengi wa watu wapotevu wanaoishi karibu na makanisa yao. Kwenye karatasi chora duara kubwa na uweke alama ya msalaba katikati ya duara. Msalaba huo unasimama mahali pa kanisa lako. Duara inasimama mahali pa eneo linalozunguka kanisa lako au eneo ambalo watu wake wangevutwa na kanisa lako. Kutoka kanisa lako mpaka penye duara ni umbali wa kilomita mbili kila upande, kwa sababu tunajua watu watahudhuria kanisa lililo na umbali wa karibu kilomita mbili.

Basi swali ndilo, “Ni watu wangapi wanaoishi ndani ya duara hiyo?” Utastaajabu kugundua ya kwamba patakuwa na watu wengi hapa zaidi ya unavyofikiria sasa! Washiriki wengi hufikiria ati panao watu mia mbili au tatu tu wanaoishi ndani ya duara inayozunguka kanisa lao. Ikiwa ni kama watu arobaini wanaohudhuria kanisani kwao wanafikiri ati wanafaulu. Kusema kweli, ikiwa eneo lako linakaliwa na wastani yapata kuwa na zaidi ya watu 1,500 waishio ndani ya duara yako na labda huenda wakawa zaidi ya idadi hiyo. Tembea kuzunguka eneo lako. Waangalie watu. Ufahamike na idadi ya watu wengi wanaoishi hapo.

Swali lifuatalo ndilo, “Ni watu wangapi kati ya hawa wangeweza kuvutwa na kanisa lako?” Yaani, ni watu wangapi kati yao wasio washiriki wa kanisa lo lote? Litakuwa jambo lisilo la kawaida ikiwa zaidi ya nusu yao ni washiriki wa makanisa mengine. Kwa hivyo, ndani ya duara inayozunguka kanisa lako kuna watu kati ya 700 na 1,000 ambao ni wapotevu. Ikiwa kanisa lako halitawatembelea, basi huenda Injili ya Kristo isiwafikie. Kwa hivyo, tunakaa kitako makanisani mwetu tukijisikia tumeridhika, tukiwa na washiriki thelathini au arobaini wakati kuna mamia ya watu wapotevu wanaoishi karibu na kanisani.

Sasa, ukifikiria idadi ya watu wengi hivyo wanaoishi ndani ya duara inayozunguka kanisa lako, yakupasa kuwa na lengo la miaka miwili kwa kanisa lako. Kumbuka, hiyo ingekuwa idadi ya watu ambao ungetarajia kujiunga na kanisa lako kwa muda huo wa miaka miwili. Lengo hilo lingekuwa halisi. Ukiweka juu sana kanisa lako litalikubali, lakini litafikiria kuwa si halisi na kwamba ni lengo lisiloweza kufikiwa. Ukiweka chini sana kanisa halitakuwa na juhudi kubwa ya kuwavuta watu hao kwa Kristo. Kwa mfano, ikiwa sasa kanisa lako lina washiriki kati ya 40 na 50, basi lengo lifaalo lingekuwa kufikisha washiriki 150 baada ya miaka miwili.

Swali lifuatalo ndilo, “Ni madarasa mangapi ya Shule ya Jumapili ambayo kanisa lako lingekuwa nayo baada ya miaka miwili ili

kuwatosheleza washiriki 150?" Ebu na tupange madarasa ya watoto. Ikiwa unao washiriki 150 wanaohudhuria kanisani, ni wangapi kati yao watakaokuwa watoto? Tungepokeza ya kuwa nusu ya idadi hiyo itakuwa watoto. Katika nchi nyingi barani Afrika nusu ya wenyeji wako chini ya umri wa miaka 14. Kwa hivyo, ukiwa na watu 150 katika Shule ya Jumapili, karibu na 75 wao watakuwa watoto wa madarasa ya Watoto Wadogo, Watoto Wakubwa na Vijana Wadogo.

Sasa hapa kunayo sheria kuhusu ukubwa wa madarasa yako. *Kusiwe kamwe na darasa lenye wanafunzi zaidi ya ishirini*. Darasa likizidi idadi hiyo mwalimu hawezi kuwaongoza watoto au kuwafundisha vema. Ikiwa darasa la watoto lina wanafunzi zaidi ya 20, ligawanye na uanzishe darasa lingine. Kwa hivyo, kama ungepanga madarasa kwa watoto 75, ungepanga uwe na madarasa manne.

Sasa na tufikirie vijana. Fikiria Kenya kama mfano. Hesabu ya watu wa nchi hii yaonyesha ya kwamba 15% ya watu wake ni wa umri wa darasa la vijana. Hiyo ina maana ya kwamba kati ya watu 150 ni idadi ya 22 ambao wangekuwa vijana. Idadi hiyo yaweza kuwa tofauti katika nchi yako, lakini ingawa ni hivyo ungepanga darasa moja la vijana.

Wanaobaki kati ya watu 150 watakuwa watu wazima. Ikiwa unao watoto 75 na vijana 22, basi ungepanga kwa watu wazima kati ya 50 na 55. Ukipanga madarasa yasiyozidi wanafunzi 20 kwa kila darasa, ungepanga madarasa matatu ya watu wazima.

Kwa hivyo, mpango wa miaka miwili tuliofikiria ni kama ifuatavyo (Kumbuka ya kwamba huu ni mfano tu. Herufi zitakuwa tofauti kwa kanisa lako, lakini fuata taratibu hiyo kwa kuweka lengo lako):

1. Tumetazama jamii na kufahamu ya kwamba kunao kama watu 800 wapotevu wanaoishi karibu na kanisa letu.
2. Lengo letu ni kuwa na washiriki 150 baada ya miaka miwili.
3. Tumepanga kuwafundisha watu hao tukiwa na madarasa 8, yaani madarasa 4 ya watoto, darasa 1 la vijana na madarasa 3 ya watu wazima.

Ni lazima tuanze sasa kupanga upanuzi wa madarasa ya Shule ya Jumapili na kuwazoeza waalimu wapya.

KUPANGA SHULE YA JUMAPILI YAKO

Tumekwisha weka lengo la miaka miwili ya Shule ya Jumapili yetu. Sasa twajua tuendako na tunalotumainia kulitimiza siku za usoni. Sasa swali ni tutaanzia wapi? Ni vizuri kuwa na lengo la kuwa na watu 150, lakini kwa sasa tunao watu 40 tu. Tunatumainia kuwa na madarasa 8, lakini sasa tunayo mawili tu. Basi, ni mipango gani tunayohitaji kupanga kuanzia sasa?

Ushike lengo la watu 150 na madarasa 8, lakini tupange kazi kuanzia mahali ulipo sasa. Makanisa mengi yanayoshindwa kuwa na Shule ya Jumapili hushindwa kwa sababu hayapangi vizuri. Huwa hayana hakika ya lengo yanalotumainia kutimiza. Huna budi kuwa na mipango utakayoifanya katika Shule ya Jumapili, na ni lazima uwe umejitayarisha kuitimiza mipango hiyo.

Ili kanisa liwe na mipango ya Shule ya Jumapili yake kunayo maswali fulani ambayo kila kanisa lingeyajibu lenyewe. Hakuna jibu moja lifaalo kwa maswali hayo. Kila kanisa litajibu swali lake kulingana na mahitaji yake na hali yake. Maswali na majibu ya kanisa yangeandikwa na viongozi wa kanisa. Viongozi hao wayachunguze mara kwa mara, kwa sababu ni mpango wa Shule ya Jumapili yao.

1. Swali la kwanza ambalo ni lazima kulijibu, *"Ni madarasa mangapi ya Shule ya Jumapili ambayo yatulazimu kuanzia nayo?"* Lengo letu ni kuwa na madarasa 8 baada ya miaka miwili, lakini hatuwezi kuanza na madarasa manane. Hatuko tayari kuwa na madarasa hayo. Tungeanzisha Shule ya Jumapili yetu na madarasa mangapi? Jibu ni rahisi. Ni lazima uwe na madarasa yasiyopungua matatu ukianzisha Shule ya Jumapili. Unaweza kuanzisha na madarasa zaidi ya hayo, lakini usiwe na chini ya hayo. Ukifanya hivi ungekuwa na darasa moja la watoto wadogo wanaotangulia umri wa shule, darasa moja la vijana wadogo na darasa moja la watu wazima. Huwezi kuwafundisha watoto wadogo pamoja na wale wakubwa. Huwezi kuwafundisha wale ambao hawajaanza shule pamoja na wale wanaojua kusoma. Hata kama unao watoto wachache ni lazima uwagawanye katika madarasa mawili, yaani darasa moja la wale wanaotangulia umri wa shule na darasa lingine la Vijana Wadogo. Na ukumbuke ya kwamba mpango huo ni wa muda tu. Huna nia ya kuendelea kuwa na madarasa ya Shule ya Jumapili hayo machache tu. Ongeza madarasa yako haraka iwezekanavyo.

Unapoanza ukumbuke ya kwamba ni lazima kila darasa liwe na mwalimu wake na mahali pake pa kukutania. Hakikisha ya kwamba

watoto wanaingia katika darasa lao kuanzia Jumapili ya kwanza. Upange mtu mzima mmoja afike mapema kuwasaidia waingie katika darasa lao. Usikubali ndugu mdogo ajiunge na dada yake mkubwa. Umshike mkono umpeleke mahali pa darasa lake lipo. Atalifurahia zaidi darasa lake na vivyo dada yake atalifurahia darasa lake.

Sasa chukua karatasi yako na uandike mpango wa madarasa utakayoanza nayo. Kwa mfano: Darasa la 1 litakuwa la watoto wanaotangulia umri wa shule, Miaka ____ hadi ____ .

Darasa la 2 litakuwa la Vijana Wadogo miaka ____ hadi ____ .

Darasa la 3 (Kama ukiwa na darasa la Vijana liandikwe hapa) Miaka ____ hadi ____ .

Darasa la 4 litakuwa la watu wazima.

2. Swali la pili ambalo ungelijibu ni *Utawapata wapi waalimu wa madarasa matatu (au zaidi)?* Hapa kuna mawazo ya kukusaidia:

A. Kwanza, fikiria washiriki wa kanisa lako ambao kuonekana wakipendezwa hasa na kazi ya Shule ya Jumapili. Ikiwa katika eneo lako kumekuwako mafundisho (Semina) ya Shule ya Jumapili, au mikutano juu ya Shule ya Jumapili, ni akina nani kati ya washiriki wa kanisa lako waliohudhuria? Mara nyingi washiriki wa kanisa hufundishwa habari za Shule ya Jumapili lakini hawatumiwi kamwe kwa kazi hiyo na makanisa yao. Kama unao washiriki wa aina hii, anza nao kuijenga Shule ya Jumapili yako.

B. Soma orodha ya majina ya washiriki wa kanisa lako kwa roho ya sala. Mara nyingi kuna majina ya washiriki ambao wangeweza kufundishwa wawe waalimu wazuri sana wa Shule ya Jumapili, lakini hawajapatiwa nafasi ya kutumika. Kumbuka ya kwamba katika kazi ya Shule ya Jumapili yakulazimu uwashirikishe washiriki wako wote wa kanisa hapo mbeleni.

C. Watafute na uombe ili Mungu akusaidie kuwatambua washiriki wa kanisa lako ambao wana kipawa cha Roho Mtakatifu cha kufundisha. Ujuzi wa elimu na kipawa cha kufundisha si lazima ziende pamoja. Mara nyingine Mungu atamtumia mtu asiye na elimu nyingi kama mwalimu mzuri wa Shule ya Jumapili.

D. Washiriki wakipatikana ambao wangukuwa waalimu wazuri wa Shule ya Jumapili, mchungaji au msimamizi wa Shule ya Jumapili aseme nao. Uwaeleze unalotaka wafanye na mambo yanayotakikana.



Uwaambie ya kwamba wanao wajibu wa kujitolea kwa kazi hii kwani sio kazi rahisi. Kama wakikubali kuifanya, basi ulete majina yao mbele ya kanisa. Ni lazima kanisa liwachague kabla ya kuanza kufundisha kwa sababu ni kanisa linalosimamia Shule ya Jumapili.

E. Waalimu hawa ni lazima wafundishwe na kuongozwa na mchungaji au mtu mwingine anayeelwa na shabaha na kazi za Shule ya Jumapili. Wachungaji wengi wanaweza kufundisha waalimu wao. Si kazi ngumu, lakini inahitaji muda mwingi.

F. Kumbuka lengo lako la miaka miwili. Kama kwa wakati huu unahitaji waalimu watatu au wanne tu, utafika wakati utakapowahitaji waalimu wanane. Ni lazima wakati wote uwe na watu wanaofundishwa wawe waalimu wa Shule ya Jumapili. Kila darasa la watoto lahitaji mwalimu msaidizi na kila darasa la vijana na la watu wazima lingekuwa na waalimu wanaofundishwa. Wasaidizi hawa wangefundishwa na waalimu mpaka wawe na ujuzi wa kuongoza madarasa yao wenyewe.

Sasa chukua karatasi yako na uendelea na mpango wa Shule ya Jumapili yako. Kwa kila darasa ulilopanga andika jina la mtu atakayekuwa mwalimu wake.

3. Swali la tatu ambalo ungelijibu ni, "Madarasa yetu yatakutania wapi?" Hili laweza kuwa tatizo, lakini, ni tatizo ambalo ni sharti kutatuliwa. Ni lazima kila darasa liwe na mahali pake pa kukutania. Kanisa lako halina budi kutafuta mahali madarasa yatakapokutania. Weka mipango kwayo.

A. Anzia kwa kuchunguza jengo la kanisa lako. Ni madarasa mangapi yanayoweza kukutania ndani kwa wakati mmoja? Itakuwaje ukiligawanya jengo la kanisa kwa pazia au mikeka? Kumbuka ya kwamba utakuwa ukifundisha Biblia katika madarasa haya. Usiweke

madarasa mawili ndani ya chumba kimoja ikiwa darasa fulani litakuwa linaimba au kucheza na kuzuia madarasa mengine yasijifunze.

B. Halafu peleeza uwanja wa kanisa lako. Je! Kuna miti mikubwa yenye uvuli ambako madarasa yangeweza kukutana chini yake?

C. Fikiria nyumba zilizo karibu, labda nyumba ya mchungaji. Ingewezekana darasa likutanie hapo?

D. Fikiria kujenga kibanda cha uvuli. Mara kwa mara unapopita barabarani utaona vibanda ambavyo vimejengwa kwa miti na nyasi. Vimejengwa na watu viwe kivuli kwa sababu ya matunda na maboga yao wanayouza. Kama wangeweza kufanya hivyo kwa biashara, kwa nini washiriki wa kanisa wasingefanya hivyo kwa kazi ya Bwana? Kata miti, nyasi au matawi na washiriki wachache wa kanisa wajenge vibanda vya madarasa kukutania.

E. Kumbuka ya kwamba utapanulisha Shule ya Jumapili yako. Lengo lako ni kuwa na madarasa manane. Labda kanisa lako lingeanza sasa kupanga kujenga vyumba zaidi vya Shule ya Jumapili. Si lazima vyumba hivyo vigarimu pesa nyingi. Washiriki wanaweza kuvijenga. Tumia miti, udongo na nyasi au vifaa vya aina nyingine ambavyo vyaweza kupatikana katika eneo lako.

Kanisa lako laweza kufanya lo lote linaloamua kufanya. Ni lazima kutatua tatizo la makao ikiwa unataka kanisa lako na Shule ya Jumapili zikue. Tumekwisha taja ya kuwa Shule ya Jumapili ni kazi ngumu. Lakini usiogope kazi hiyo!

Sasa chukua karatasi yako na uendelee kuandika mpango wa Shule ya Jumapili yako. Chini ya jina la mwalimu wa kila darasa andika mahali darasa hilo litakapokutania.

4. Swali la nne ambalo ungelijibu ni, "Ni saa ngapi Shule ya Jumapili yetu itakapokutania?" Ni jambo muhimu kupanga saa na kuutangaza ili kila mmoja afahamu. Kwa kawaida wakati wa Shule ya Jumapili kukutana ni saa moja kabla ya ibada ya siku ya Jumapili. Ungepanga mkutano wa Shule ya Jumapili uwe saa iliyo nzuri kwa watu wa kanisa lako na jamii. Jaribu kuweka mipango ili madarasa yote yakutane wakati mmoja. Kumbuka ya kwamba tunataka watu wa jamaa nzima wafike Shule ya Jumapili pamoja. Hapa kuna mawazo ya kukusaidia juu ya saa:

A. Anza Shule ya Jumapili saa moja kabla ya ibada haijaanza.

B. Anza bila kuchelewa. Mchungaji au kiongozi wa Shule ya Jumapili apige kengele au kugonga kipande cha chuma ili

kuwafahamisha watu ya kwamba saa ya Shule ya Jumapili imeanza. Mara nyingi tunasikia msemu usemao ati Afrika hatuna masaa. Lakini hiyo si kweli. Watoto huenda shule saa ya kawaida. Watu hufika kazini saa ya kawaida. Hata tunaingia ndani ya gari la moshi au basi (motokaa) saa ya kawaida. Tunaweza, tena ni lazima, tuanze Shule ya Jumapili saa ya kawaida. Kama usipoanza Shule ya Jumapili saa ya kawaida utachelewa kuanza ibada saa ya kawaida na akina mama watachelewa kurudi nyumbani kutayarisha chakula kwa jamaa zao.



C. Maliza saa ya kawaida. Shule ya Jumapili isichukue muda uzidio saa moja. Tangaza Shule ya Jumapili itaanza saa ngapi na itamalizika saa ngapi. Piga kengele au gonga ngoma kuonyesha ya kuwa saa ya Shule ya Jumapili imekwisha, na waalimu waruhusu wanafunzi kuondoka waingie ibada.

Sasa chukua karatasi yako na chini ya mipango yote ya darasa, andika saa kanisa lako litaanzisha Shule ya Jumapili na saa ya kumaliza Shule ya Jumapili.

5. Swali la tano ambalo ungelijibu ni, “Ni vitabu vipi vya masomo utakavyotumia, na utavipataje?” Kwa maana kitabu hiki kimeandikwa ili kitumiwe katika makanisa ya Kibatisti, inadhaniwa ya kwamba makanisa yatumia vitabu vya masomo ambavyo vimechapishwa na Baptist Publishing House. Anwani za nyumba hizi za “publishing” zitaandikwa upande wa nyuma wa kitabu hiki. Vitabu hivi vimeelezwa kwa kirefu katika Sura ya 3. Ungeandika kwa Publishing House yako ili upewe maelezo zaidi juu ya vitabu hivi, bei yake na jinsi uwezavyo kuviagiza. Kumbuka ya kwamba ni lazima kuviagiza kabla ya muda usiopungua miezi miwili kabla ya kuvihitaji vitumike. Hivyo utakuwa na hakika kuvipata kwa wakati ufao.

Sasa chukua karatasi yako ya mpango na andika anwani ya Publishing House, hesabu ya vitabu utakavyohitaji kwa kila darasa, na tarehe ya kuagiza vitabu vijavyo ili usije ukajikuta huna vitabu wakati ule unapovihitaji.

6. Swali la mwisho ambalo ungelijibu ni, “Watoto wakipata umri wa kutosha waingie darasa lifuatalo, utawahamishaje kutoka darasa moja hata lingine?” Kwa mfano, ikiwa darasa lina watoto wadogo hadi ya miaka saba na mtoto amefikisha miaka minane, utafanyaje umpandishe kwa darasa la Watoto Wakubwa? Usikubali wapandishwe wanaposherehekea siku yao ya kuzaliwa. Jambo hilo litamchanganyisha

mwalimu na wengi wa watoto. Kunao taratibu. Labda ungependelea kuifuata kanisani mwako.

A. Tenga Jumapili ya kwanza kila Januari iwe siku maalum ya Shule ya Jumapili kanisani mwako. Waweza kuiita Siku ya Kupandishwa Madarasa, kwani hii ni siku ya watoto wote ambao wamefika umri wa kutosha watahamishwa juu kutoka darasa moja hadi darasa lifuatalo.

B. Jumapili hiyo wakati wa ibada, watoto wote wa madarasa mbalimbali waketi upande mmoja kanisani. Waketi darasa kwa darasa pamoja na waalimu wao. Wazazi wangekaa upande mwingine kanisani. Kama kunao watoto ambao wazazi wao, kwa kawaida, hawaji kanisani, hakikisha ya kuwa siku hiyo wamealikwa kuhudhuria ibada hii maalum.

C. Mchungaji angetoa maelezo juu ya Shule ya Jumapili ya kanisa. Angewajulisha waalimu wote wa kanisa na hasa kutia mkazo ya kwamba kunayo madarasa ya Biblia kwa wazazi vile vile.

D. Halafu mchungaji angeita darasa la Watoto Wadogo. Watatembea mbele ya mkutano pamoja na mwalimu wao na kusimama mbele ya mkutano. Mwalimu anaweza kueleza kwa kifupi juu ya darasa, umri wa watoto na kazi wanayofanya. Halafu wanafunzi wapewe nafasi ya kuimba na kukariri vifungu vya Biblia.

E. Halafu mchungaji awashukuru watoto na kueleza wazazi ya kwamba wachache wa watoto hao wamemaliza mafundisho ya darasa hilo na wamefika umri wa kupandishwa kuingia darasa lifuatalo. Angeita majina ya wale wanaopandishwa na kumpatia kila mmoja wao "Cheti cha Kupandishwa Juu" ambacho kimeandikwa jina lake na kutiwa sahihi ya mchungaji, msimamizi wa Shule ya Jumapili na mwalimu wa darasa alilomaliza. Vyeti hivi vyaweza kupatikana katika Baptist Publishing House.

F. Mchungaji angerudia taratibu hiyo kwa kila darasa la watoto. Watoto warudipo kwa viti vyao wakiwa na vyeti watakuwa wamejawa na furaha, wazazi wao watakuwa na furaha na kila kitu kitakuwa kimefanyika kwa taratibu njema. Umeufuata mpango! Lakini kumbuka, ni watoto wanaopandishwa tu watakaopewa vyeti. Wengine watangojeka mpaka watakapofikia umri wa kupandishwa kabla ya kupatiwa vyeti vyao.

Kwa hivyo sasa unao mpango wa Shule ya Jumapili yako. Tena unalo lengo la miaka miwili linalotazamia upanuzi mkubwa. Basi swali ndilo, "Utatokaje ulipo sasa hata ufikie mahali umehamu kufikia baada ya miaka miwili?" Kunayo kazi nyingi ngumu ya kufanywa. Labda tunaweza kukusaidia kuona njia.

KUTUMIA SHULE YA JUMAPILI KUWAFIKIA WATU

Shabaha ya Shule ya Jumapili ni kuwatayarisha na kuwatuma washiriki wa kanisa ili wawavute jamii. Unaweza kujenga kanisa lako kwa njia ya Shule ya Jumapili. Kulijenga kanisa siyo kujenga kuta na paa. Kanisa ni watu. Watu wasio Wakristo wanaishi karibu na makanisa yetu. Swali ndilo “Twaweza kuwafikiaje?” Swali hilo laweza kujibiwa kwa neno moja, *Kuwatembelea*.

Madarasa ya Shule ya Jumapili yanaweza kusimamiwa yafanye kazi ambayo matokeo yake yataleta manufaa makubwa. Kazi hiyo ni ya *kutembelea*. Hii ni kazi ambayo kila mwanafunzi wa Shule ya Jumapili anaweza au angeshirikishwa kuifanya.

Waalimu wa Shule ya Jumapili hawana budi kutembelea. Haidhuru wawe waalimu wa watoto wadogo au wa watu wazima ni lazima kutembelea. Waalimu wa madarasa ya watu wazima na vijana wangependelea wanafunzi wa madarasa yao kutembelea na kuwaongoza katika kazi hii. Kazi ya darasa la Shule ya Jumapili iliyo muhimu zaidi ni kutembelea. Lazima watembelee:



1. Wanafunzi wa darasa. Mwalimu hasa yampasa awajue kila mwanafunzi wa darasa lake kwa jina lake, jamaa yake na hali ya maisha yake binafsi.
2. Wanafunzi wa darasa ambao hawahudhuria. Wangewatembelea ili wajue shida walizo nazo na kujaribu kuwarudisha.
3. Washiriki wa kanisa ambao hawahudhuria Shule ya Jumapili. Wahimizwe waje na kushiriki katika mafundisho ya Biblia.
4. Wakristo wa eneo lao ambao hawahudhuria kanisa lo lote. Labda hawangependelea kujiunga na kanisa la Kibatisti lakini wangependelea

kuhudhuria masomo ya Shule ya Jumapili na kufurahia ushirika wa Kikristo.

5. Watu wasio Wakristo. Wawatafute. Wawafahamu. Wawaalike kwa masomo ya Biblia. Wawavute kwa Kristo. Kama darasa la Shule ya Jumapili likifanya kazi, kila Jumapili mwalimu anapofundisha kutakuweco watu wasio Wakristo kujifunza somo hilo.

Jambo la umuhimu ni kupanga wakati wa kutembelea. Mwalimu angetenga wakati fulani kila wiki kutembelea. Ni lazima ahakikishe ya kwamba vikundi tofauti vya darasa lake vimepanga wakati wao wa kutembelea. Kumbuka ya kuwa kazi ambayo haipangwi vizuri haiwezi kutendeka vizuri. Kama mwalimu hapangi jinsi ya kutembelea, hatatembelea wala washiriki wa darasa lake hawatatembelea. Moja ya kazi muhimu zinazofanywa na mwalimu ni kuwaleta watu kwa Kristo. Asisahau jambo hili.

Ufuatao ni mpango unaoweza kufuata kwa Shule ya Jumapili yako ili kutengeneza jinsi madarasa yako yawezavyo kutembelea na kuwavuta watu kwa Kristo na kanisa. Mpango sio kamili. Kunayo matayarisho unayohitajika kuyafanya kwa kikamilifu kanisani mwako ili mpango ufuatane na mahitaji ya eneo lako. Bali nia yenyewe itakuweshesha kufanya kazi ikiwa utafuata.

Kwanza, Mchungaji angekutana na walimu wa madarasa ya Shule ya Jumapili ya watu wazima na vijana. Angewaeleza walimu shabaha na kazi za Shule ya Jumapili. Ni lazima mwalimu aelee ya kuwa moja ya kazi za Shule ya Jumapili ni kuwavuta watu kwa Kristo. Mchungaji atamweleza kila mwalimu jinsi ya kutembelea na kushuhudia. Angekuwa akienda pamoja na mwalimu wakati mwenyewe anapotentembelea. Mwalimu atapeleleza mpaka aelee jinsi ya kuingia ndani ya nyumba na kuanzisha mazungumzo na watu juu ya darasa la Biblia na kuwaalika wahudhurie. Atajifunza jinsi ya kuwatolea ushuhuda wake na kumshuhudia Kristo.

Pili, baada ya mwalimu kufahamu jinsi ya kutembelea angeendelea na kutembelea. Atakuwa na kitabu cha kuandika majina ya watu anaokutana nao ambao si Wakristo au hawahudhuria kanisa. Kando ya kila jina ataandika anwani au maelezo ya kumweshesha kufikia nyumba ya mtu huyo. Orodha ya majina hayo itaongezeka kila wakati anapotentembelea.

Tatu, atagawanya wanafunzi wa darasa lake katika vikundi vidogo vya watu watano watano. Kama ana wanafunzi kumi, atawagawanya vikundi viwili. Ni lazima agawe vikundi kwa uangalifu, akihakikisha ya

kwamba kila kikundi kinao wanafunzi imara, waaminifu na ya kwamba wale washiriki dhaifu wangepawanywa kati ya vikundi hivyo viwili.

Nne, mwalimu atamchagua mmoja na washiriki wa kila kikundi awe kiongozi wa kikundi chake. Viongozi wa vikundi wangukuwa washiriki waaminifu. Kama vile mchungaji alivyomfundisha mwalimu kutembelea, vivyo hivyo mwalimu atawafundisha viongozi wa vikundi jinsi ya kutembelea. Mwalimu atawaeleza viongozi wa vikundi shabaha ya Shule ya Jumapili na jinsi iwezavyo kuwasaidia kulijenga kanisa lao na kuwaleta watu kwa Kristo. Mwalimu atawaeleza viongozi wa vikundi ya kwamba wana wajibu wa aina mbili. Wa kwanza ni kuwasimamia na kuwatumikia wale washiriki wanne wa vikundi vyao. Kama mmoja wao hayupo kiongozi angetafuta ni kwa nini hayupo. Kama kunalo tatizo angemwelezea mwalimu wake. Wajibu wa pili ni kuwafundisha washiriki wa vikundi vyao jinsi ya kutembelea kama vile walivyofundishwa na mwalimu wao.

Tano, angempatia kila kiongozi wa kikundi majina mawili ya watu wasio Wakristo ambao wako katika orodha yake. Halafu aeleze ya kwamba ni wajibu wa kila kikundi kuitembelea nyumba hizo mbili wiki hiyo. Kiongozi wa kikundi atawachagua kati ya washiriki wake wale watakaotembelea nyumba ya kwanza. Kumbuka, huyu ni mtu mpotevu ambaye amekwisha tembelea na mwalimu. Washiriki wangesema naye juu ya darasa lao la masomo ya Biblia. Wamweleze jinsi walivyosaidiwa na masomo hayo katika maisha yao. Wangempasha ushuhuda wao jinsi Kristo alivyowafanyia. Kabla ya kuondoka nyumbani humo, wataongoza katika maombi mafupi. Kama kunao watoto nyumbani humo maelezo hayo yangepashwa kwa waalimu wa madarasa ya watoto. Siku nyingine kiongozi wa kikundi atatuma washiriki wale wengine wa kikundi chake kutembelea nyumba ya pili na kupeleka ujumbe ule ule. Kiongozi wa kundi awe mwangalifu kuona kwamba kila mwanafunzi wa kikundi chake anatembelea.

Sita, kama kutembelea kunavyoendelea, watu wengi zaidi wangeweza kuhudhuria darasani. Mwalimu atalazimika kuanzisha vikundi vipya. Atajaribu kukifanya kila kikundi kiwe na wanafunzi watano au sita. Kianzishwapo kikundi kipya labda itamlazimu mwalimu kubadilisha vikundi vyote, kwani hangewaweka pamoja wanafunzi wapya katika kikundi kimoja. Awaunge wanafunzi wa zamani na wanafunzi wapya. Wakati wote wachague washiriki waaminifu na wenye ujuzi kuwa viongozi wa vikundi. Hakikisha umemweleza kiongozi wa kila kikundi analotakiwa kulifanya.

Saba, kumbuka ya kwamba pasiwe na darasa lenye wanafunzi zaidi ya 20. Kama vikundi vyako vinafanya kazi haitachukua muda mrefu

kabla ya kuwa na wanafunzi zaidi ya 20. Mwalimu, mchungaji na kiongozi wa Shule ya Jumapili wangepanga kuligawanya darasa. Usiogope kuligawanya darasa lako. Hii ndiyo njia inayoweza kuisaidia Shule ya Jumapili yako ikue. Mwalimu wa kila darasa angekuwa akimfundisha mwalimu mwingine mpya. Angekuwa akipatiwa nafasi ya kufundisha mara kwa mara. Mwalimu angemfundisha kazi zote zinazofanywa na mwalimu wa Shule ya Jumapili, ili darasa likiwa tayari kugawanywa pawe na mwalimu tayari wa kuanzisha darasa jipya.

Nane, baada ya kugawanya madarasa, kila mwalimu anangepanga darasa lake katika vikundi na kuvituma kutembelea. Sasa, kanisa lako lina madarasa mawili yakifanya kazi badala ya darasa moja na Shule ya Jumapili yako itaendelea kukua. Kumbuka ya kwamba mpango wako wa miaka miwili ulikuwa na lengo la madarasa manane. Sasa umekwisha ongeza darasa moja jipya na labda madarasa ya watoto au vijana yanaweza kugawanywa pia. Hii ndiyo njia itakayokufikisha kwa lengo lako.

Kama Shule ya Jumapili yako inakua, kanisa lako pia litakua. Watu wasio Wakristo watakuwa wakihudhuria madarasa. Watasikia Biblia ikifundishwa. Watasikia Injili ikihubiriwa. Kwa njia ya ushuhuda na maisha ya mwalimu na washiriki wa darasa wengi wao watampokea Kristo. Kwa hivyo Shule ya Jumapili inalijenga kanisa.

Kunalo jambo lingine muhimu. Utaona ya kwamba kazi yote ya Shule ya Jumapili inahusika na siku ya Jumapili. Wakati mwingine jumuiia ndogo ya makanisa au ushirika wa makanisa katika eneo fulani utapanga mikutano maalum siku ya Jumapili. Makanisa mengine hayatakutana siku hiyo au yatakuwa na ibada mapema asubuhi ili washiriki wote waweze kwenda katika kanisa lingine kwa ushirika. Je, unaweza kufikiri kitu ambacho kingetendeka ikiwa watu waliotembelewa katikati ya wiki wangefika kanisani Jumapili na kukuta milango imefungwa? Jumapili ndiyo siku ya muhimu zaidi ya wiki ya kanisa. Kazi zote za kanisa zahusika na Jumapili. Hilo ni jambo la kweli hasa kwa Shule ya Jumapili. Uyaongoze makanisa ya eneo lako yawe yakipanga mikutano maalum Jumamosi au siku nyingine yo yote ya wiki. Jumapili ni ya mikutano ya kanisa mahali pake. Kama kunao mkutano maalum kwa mfano kufunguliwa kwa kanisa au kuweka wakfu, tuma ujumbe wa washiriki wawili au watatu kutoka kanisa lako. Bali kanisa lenyewe ni lazima liendeshe shughuli zake za kawaida kila Jumapili.

MWALIMU WA SHULE YA JUMAPILI

Ushirika wa wakulima ulinunua tingatinga la bei kubwa ili liwasaidie kulima mamia ya ekari zao za ardhi. Walipanga kwa uangalifu kile watakachopanda, mstari watakaofuata na aina ya mbegu watakazozitumia. Walijua tarehe ya kupanda, siku ya kuweka mbolea na kiasi cha mvua ambacho kilihitajika. Walikuwa

wamepanga kwa makini na kujitayarisha vema. Walikosea kufikiria kitu kimoja tu. Wakati huo au baadaye wangehitaji mwendeshaaji wa tingatinga na kati yao hakuna aliyejua kuliendesha hilo tingatinga. Ni jambo la muhimu kupanga kwa makini Shule ya Jumapili na kujitayarisha kwa njia ifaayo. Ni jambo la muhimu kuelewa



shabaha na kazi za Shule ya Jumapili na mambo ambayo ingetimiza kanisani mwako. Lakini pamoja na mipango yako yote, wakati huu au baadaye mwendeshaaji wa tingatinga atahitajika; mtu ambaye anaweza kutimiza mipango yote. Hiyo ni kazi ya mwalimu wa Shule ya Jumapili. Katika kazi ya Shule ya Jumapili, waalimu wema waliofundishwa wanahitajika kabisa.

Kitabu hiki si cha kuwafundisha waalimu jinsi ya kufundisha. Tungependa, hata hivyo, kujaribu kuyajibu maswali kadhaa na kupeana mwongozo ambao ungekuwa wa manufaa kwa makanisa na waalimu kuhusu kazi hii ya muhimu.

1. Ni mtu wa tabia gani ambaye kanisa lingemchagua awe mwalimu wa Shule ya Jumapili?

A. Jambo la kwanza ambalo kanisa lingetazamia ni awe mshiriki wa kanisa mwaminifu. Kama yeye si Mbatisti asikubaliwe kabisa. Akiwa ni Mbatisti lakini hajajiunga na kanisa hilo, tafuta sababu kwanza kabla hajachaguliwa kufundisha. Mwalimu wa Shule ya Jumapili lazima alipende kanisa lake na awe mwaminifu kwalo. Hii ina maana ya kwamba anahudhuria mikutano ya kanisa na kulisaidia kwa kila njia awezayo. Je, Mtu yule anayefikiriwa ni mshiriki mwaminifu? Je, Analipenda kanisa lake?

B. Jambo la pili ambalo kanisa lingefikiria ni kama kwamba yeye ni mtu anayefuata kanuni za maisha ya Kikristo. Je, Washiriki wa kanisa wanamwamini? Je, ni mpatanishi wa amani? Je, Anaheshimiwa kijijini, au anao udhaifu na dhambi maishani mwake ambazo zingewafanya watu wasio Wakristo kujiepusha na darasa lake la masomo ya Biblia? Ni lazima mwalimu wa Shule ya Jumapili awe mtu ambaye anaonyesha kwa tabia yake ya kwamba ni Mkristo.

C. Ni lazima awe akilitegemeza kanisa lake kwa matoleo yake. Ni lazima viongozi wa kanisa wawe vielelezo katika kutoa zaka. Jambo hili lawahusu waalimu wa Shule ya Jumapili. Je, Anawezaje kufundisha Biblia wiki baada ya wiki ikiwa hana nia ya kutenda yale yanayofundishwa na Biblia juu ya matoleo?

D. Ni lazima awe mtu wa kiroho akimwabudu Bwana kanisani na nyumbani kwake. Kama si wa kiroho, asipewe kazi ya kuyaongoza maisha ya kiroho ya watu wengine.

E. Katika mafundisho yake kutaonekana dalili ya kwamba amepewa kipawa cha kufundisha na Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuzitaja dalili hizi zote, lakini tazama dalili zifuatazo:

Je, anaweza kufundisha? Je, watu wanafurahia mafundisho yake? Je, maisha ya wanafunzi wake yanabadilishwa na mafundisho yake? Je, juhudi zake zinazaa matunda ya kiroho? Mtu huenda akawa mshiriki na Mkristo mzuri wa kanisa, lakini ikiwa hajapewa kipawa cha kufundisha hawezi kufaulu kazini mwake. Hili si kosa lake, bali ina maana ya kwamba Mungu ana kazi nyingine ambaye anamtaka afanye. Katika kufikiria waalimu kanisa lisiwatafute watu ambao ni wakamilifu katika kila moja ya mambo hayo tuliyotaja kabla ya kuwachagua kufundisha. Hata hivyo, mtu angeonekana ya kwamba anafanya juhudi ya kuyatimiza na awe na bidii ya kujitoa mwenyewe aendelee kukua kwayo.

2. Kwa kawaida, kazi za mwalimu wa Shule ya Jumapili ni nini? Wajibu wake ni nini, ili kanisa pamoja naye waweze kufahamu kama akifanya kazi anayokusudiwa kuifanya au la?

A. Darasa lake linapokutana ni lazima awe amejitayarisha kulifundisha Neno la Mungu kwa usahihi.

B. Ni lazima atembelee, na kulingana na umri wa wanafunzi wake yamlazimu kuwapanga ili watembelee.

C. Ni lazima awe akihudhuria wakati wote. Kama atachelewa ni lazima amfahamishe mapema kiongozi wa Shule ya Jumapili au

mchungaji. Ni lazima ahakikishe ya kwamba kunaye mtu mwingine wa kufundisha darasa lake kama hatafika.

D. Ni lazima kuwahi mapema kama dakika kumi na tano Jumapili asubuhi ili kutayarisha mahali ambapo darasa lake litakutania, na kuwasalimia wanafunzi wake wafikapo. Asingojee mpaka saa ya Shule ya Jumapili ifike ndipo aanze kuchukua viti kupeleka darasani mwake.

E. Ni lazima kuhudhuria mikutano ya mafundisho ambayo itamsaidia kuwa mwalimu thabiti zaidi. Ni lazima aendelee na kujaribu kuimarisha ujuzi wake wa kufundisha.

F. Ni lazima awajue wanafunzi wake na kujitolea kuwasaidia.

G. Mwisho, ni lazima awe tayari kuwavuta watu kwa Kristo.

3. Je, Ni malengo gani ya kibinafsi ambayo mwalimu wa Shule ya Jumapili angekuwa nayo? Ni jambo muhimu kujua jinsi watu wengine wanavyotumainia mwalimu wa Shule ya Jumapili awe na afanye. Lakini pia ni jambo la muhimu vile mwalimu wa Shule ya Jumapili mwenyewe anavyojitumainia. Ni lazima kuwe na kujitolea moyoni mwake ili aweze kupendelea awe yote awezayo kuwa na kuyatimiza yote awezayo kwa utukufu wa Mungu. Hatuwezi kuyataja yote ambayo mwalimu angeyatumainia binafsi lakini hapa kunayo machache:

A. Kabla ya jambo lingine lo lote, mwalimu mwenyewe atakuwa ana hakika kwamba ameokolewa na ya kwamba Yesu Kristo kwa kweli ni Bwana na Mwokozi wake. Ikiwa hana uhakika huo hana jambo la kufundisha.

B. Ni lazima mwalimu awe mwanafunzi wa Biblia. Ni lazima kuisoma, kuiweka moyoni mwake na kuishi maisha yake kuyatii mafundisho yake.

C. Ni lazima mwalimu wa Shule ya Jumapili awe Mkristo anayeomba sana. Ni lazima kutenga muda fulani kila siku wa kuwa pekee akiomba. Ni kwa njia ya maombi, "atakaa ndani ya Kristo" (Yohana 15:5) na kuweza kuwa na ushirika naye. Ni kwa njia ya maombi ya kwamba anatubu dhambi zake na kuuliza neema ya Mungu,



upendo na uwezo maishani mwake. Ni lazima mwalimu ajifunze jinsi ya kuomba kwa uwezo wa Mungu wa kuyaokoa maisha ya wale aliowatembelea wasio Wakristo. Ni lazima mwalimu wa Shule ya Jumapili awe mtu wa maombi.

D. Ni lazima mwalimu wa Shule ya Jumapili aishi maisha ya uteule. Ni lazima pawe na tofauti kati ya maisha yake na maisha ya watu ambao si Wakristo. Paulo aliwaambia Wakristo wa Efeso, "Msienende kama Mataifa (wasio Wakristo) waendavyo" (Waefeso 4:17). Jambo hilo ni la kweli hasa kwa mwalimu wa Shule ya Jumapili. Maisha yake yangukuwa kielelezo kwa wengine katika mambo yote. Upendo na furaha ya Bwana vingonekana katika kila jambo atendalo.

Mwalimu wa Shule ya Jumapili angekuwa amejitoa binafsi ili kuwavuta watu kwa Kristo. Jambo hili limetajwa kuwa ni kazi ya mwalimu wa Shule ya Jumapili. Ni lazima liwe jambo la kujitolea kati yake na Bwana. Wakati utafika ambapo atakuwa akipiga magoti akiomba, "Mungu akiwa msaidizi wangu, nitalifanya." Kwa kupeleleza malengo manne yaliyotajwa hapa juu angekuwa wakati wote mtu ambaye anaweza kutumiwa na Roho Mtakatifu kwa kazi hii ya muhimu.

4. Je, mwalimu wa Shule ya Jumapili anajitayarisha namna gani kufundisha Jumapili asubuhi? Hiki si kitabu cha taratibu za kufundisha, lakini hapa pana mawazo ya kusaidia kufanya matayarisho:

A. Usisahau ya kwamba kazi ya Bwana ni lazima ifanywe kwa uwezo wa Bwana, ila sivyo haitafaulu. Kabla ya kufanya jambo lo lote, ni lazima kujitayarisha mwenyewe kiroho.

B. Anza matayarisho yako mapema wakati wa wiki labda Jumatatu. Uwe na wiki nzima kusoma na kupeleleza vifaa kufundishia, kutafuta mifano na kufikiria jinsi uwezavyo kuyafanya mafundisho yafurahishe. Mwalimu ambaye hawezi kujitayarisha hadi Jumamosi hatakuwa na mambo mengi ya kufundisha Jumapili asubuhi.

C. Ujifunze kuvitumia vitabu vya mwalimu na vitabu vya masomo. Jambo hili litahitaji mazoezi na masomo, lakini vitabu hivi ni vyombo ambavyo ni lazima kuvitumia kama ungefundisha kwa mafanikio.

D. Kumbuka ya kwamba kusudi lako silo kumaliza muda wa saa moja tu Jumapili asubuhi. Yawalazimu wanafunzi walishwe na Neno la Mungu. Fanya mafundisho yako rahisi; tumia maneno ambayo yataeleweka na wanafunzi wako. Pambana wiki baada ya wiki na tatizo la jinsi uwezavyo kuueleza ukweli wa somo uingie katika fikira za washiriki wa darasa lako.

E. Unaweza mara kwa mara kuangalia kitabu chako cha masomo, lakini usikisome darasani. Uelewe jambo utakalofundisha. Uwaangalie wanafunzi wako unapofundisha. Unaweza kufahamu kutoka nyuso zao kama wanapendezwa na kuelewa na jambo unalolifundisha.

F. Ni lazima usadikishwe moyoni mwako na ukweli wa jambo unalolifundisha.

G. Kumbuka ya kwamba hujafundisha halisi mpaka kuwe na mabadiliko katika maisha ya wanafunzi. Thibitisho la mafundisho ni kukua kwa wanafunzi.

Wewe kama mwalimu wa Shule ya Jumapili una nafasi kubwa na wajibu wa sifa hali ya juu mno ulimwenguni: ni kufundisha Neno la Mungu. Kazi yako ni kuwaongoza watu kufahamu ukweli wa kiroho na kukata shauri ya maishani mwao kwa ajili ya Kristo. Usiruhusu jambo lo lote likuzuie kufanya vema iwezekanavyo katika wajibu wako huu mkuu.



Kwa vifaa zaidi na maelezo waulize wagawanyaji wa vifaa wanaoitumikia nchi yako:

**Baptist Publishing House
Box 228
Lobatse, Botswana**

**Baptist Publications House
Box 30370
Nairobi, Kenya**

**Baptist Publications
Box 444
Lilongwe, Malawi**

**Baptist Literature Centre
Box 1240
Moshi, Tanzania**

**Baptist Bookshop
Box 1734
Kampala, Uganda**

**Baptist Publishing House
Box 31995
Lusaka, Zambia**

**Baptist Publishing House
Box 8241 Belmont
Bulawayo, Zimbabwe**